TAARIFA YA MWAKA YA BARAZA LA MADIWANI IKIELEZEA UENDESHAJI NA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

TAARIFA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI YA UENDESHAJI NA UWAJIBIKAJI KIPINDI CHA KUISHIA TAREHE 30 JUNI, 2017

UTANGULIZI

Halmashauri yetu ina ina ukubwa wa kilometa za mraba 6,419 na mwaka huu ina jumla ya watu 177,346. Wilaya ina tarafa 3, kata 20, vijiji 62 na vitongoji 236. Makao makuu ya Wilaya yapo katika mji wa Monduli. Wilaya ina jimbo moja la uchaguzi, ina Mbunge 1 na madiwani 27. Madiwani wakuchaguliwa ni 20 na wa viti Maalumu ni 7.
Mipango ya Halmashauri imeendelea kujikita katika kutimiza Dhamira ya Halmashauri ya kutekeleza Dira, Kauli Mbiu na Utekelezaji Malengo ya Halmashauri ya 2015/2016 na mpango wa mwaka unaofuata.

UENDESHAJI WA HALMASHAURI (VIKAO VYA KISHERIA NA USIMAMIZI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA HALMASHAURI)

Uendeshaji wa Halmashauri

Baraza la Madiwani liliundwa baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015 baadaye Baraza la Madiwani liliunda Kamati za Kudumu 4 (Fedha Utawala na Mipango, Huduma za Jamii, Uchumi Ujenzi & Mazingira na Kamati Shirikishi ya Kudhibiti UKIMWI, Kamati ndogo ya Ardhi na Kamati Ndogo ya Maadili, Kamati Ndogo ya Mfuko wa Jimbo). Katika ngazi ya Kata shughuli za maendeleo zilisimamiwa na Kamati za Maendeleo ya Kata (WDC) kwa utaratibu ule ule wa vikao kama ilivyo ngazi ya wilaya. Kamati hizi zilitekeleza wajibu wake kwa kufanya vikao vya kisheria kwa mwaka huu kama ifuatavyo:-

VIKAO VYA KISHERIA

NGAZI YA KATA.

Katika ngazi ya kata, Halmashauri ilisimamia utekelezaji wa malengo na kuhakikisha ufanisi wa mtiririko wa taarifa kushuka ngazi za vijiji na kupeleka ngazi ya wilaya kupitia vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata (WDC). Vikao hivi vilifanyika katika kata kama ifuatavyo:-

KATA	MIKUTANO YA WDC ILIVYOPASWA KUFANYIKA	MIKUTANO YA WDC ILIVYOFANYIKA	% YA UTEKELEZAJI	MAELEZO
MONDULI JUU	4	4	100	Mikutano imefanyika kama ilivyokusudiwa
ENGUTOTO	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
MONDULI MJINI	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
MESERANI	4	4	100	Vikao vilifanyika kama

				ilivyopangwa
MOITA	4	3	75	Kiako kimoja hakikufanyika ilivyokuwa imekusudiwa sababu ni kukosekana kwa akidi
LOLKISALE	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
SEPEKO	4	3	75	Kiako kimoja hakikufanyika ilivyokuwa imekusudiwa sababu ni kukosekana kwa akidi
LEPURKO	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
MAKUYUNI	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
MSWAKINI	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
ESILALEI	4	3	75	Kiako kimoja hakikufanyika ilivyokuwa imekusudiwa sababu ni kukosekana kwa akidi
MTO WA MBU	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
MAJENGO	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
SELELA	4	3	75	Kiako kimoja hakikufanyika ilivyokuwa imekusudiwa sababu ni kukosekana kwa akidi
ENGARUKA	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
LEMOOTI	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
LASHAINE	4	3	75	Kiako kimoja hakikufanyika ilivyokuwa imekusudiwa sababu ni kukosekana kwa akidi
MIGUNGANI	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa

NAALAMI	4	4	100	Vikao vilifanyika kama ilivyopangwa
MONDULI MJINI	4	3	75	Kiako kimoja hakikufanyika ilivyokuwa imekusudiwa sababu ni kukosekana kwa akidi baada ya wenyeviti 3 wa vitongoji kuondolewa udhamini wa chama kilichowadhamini.

NGAZI YA HALMASHAURI YA WILAYA

KAMATI	**VILIVYOPASWA**	**VIKAO VILIVYOFANYIKA**	**% YA UTEKELEZAJI**	**MAELEZO**
Baraza la Madiwani	6	6	100	Vikao vimefanyika kama ilivyopangwa
Fedha Utawala na Mipango	14	14	100	Vikao vya dharura vimeongezeka kutokana na mabadiliko ya ratiba ya bajeti na masuala mengine ya kitaifa
Huduma za Jamii, Elimu, Afya na Maji	4	5	125	Vikao vimekuwa vikifanyika na kuleta tija ya Maendeleo kwa Halmashauri
Uchumi Ujenzi & Mazingira	4	4	100	Vikao vimefanyika kama ilivyopangwa
Kamati ndogo ya Ardhi	4	4	100	Vikao vimefanyika kama ilivyopangwa
Kamati Ndogo ya Maadili	4	0	0	Hakuna hoja iliyowasilishwa
Kamati ya Mfuko wa Jimbo	1	1	100	Kikao kilifanyika kama kilivyopangwa
Timu ya Menejimenti (CMT)	12	15	125	Vikao vimekuwa vikifanyika na kuleta tija ya Maendeleo kwa Halmashauri

USIMAMIZI NA UTAWALA

Aidha Halmashauri imeendelea kuwa na Idara 13 na Vitengo 6 vyenye jumla ya Wakuu wa Idara 19, miongoni mwao kitengo kimoja hakina Mkuu wa nafasi hiyo kama ifuatavyo:-

Na.	IDARA	MKUU WA IDARA	KAIMU MKUU WA IDARA	MAELEZO
1.	Utumishi na Utawala	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea
2.	Fedha na Biashara (DT)	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea
3.	Mipango, Ufuatiliaji na Takwimu	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea
4.	Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani	1		Kitengo na kazi za kitengo zinaendelea vizuri
5.	Kitengo cha Sheria	1		Kazi za kitengo zinaendelea vizuri
6.	Kitengo cha Uchaguzi	1		Kazi za kitengo zinaendelea vizuri
7.	Kilimo na Umwagiliaji	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
8.	Mifugo na Uvuvi	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
9.	Ujenzi	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
10.	Maji	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
11.	Elimu Sekondari	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
12.	Elimu Msingi	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
13.	Ardhi na Maliasili	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
14.	Kitengo cha Nyuki		Amestaafu	Taratibu zinaendelea za kumpata mkuu wa kitengo
15.	Maendeleo ya Jamii	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
16.	Afya	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea vema
17.	Kitengo cha manunuzi	1		Kazi za kitengo zinaendelea vizuri
18.	Kitengo cha Teknolojia habari na Mawawasiliano	1		Kazi za kitengo zinaendelea vizuri
19.	Idara ya Mazingira na Usafi wa Taka Ngumu		Amehama	Taratibu zinaendelea za kumpata mkuu wa kitengo
Idara Saidizi				
20.	TSC		1	Ameteuliwa kukaimu
21.	Ukaguzi wa Shule za Msingi	1		Idara na kazi za kiidara zinaendelea

UKUSANYAJI MAPATO YA NDANI

Ukusanyaji mapato umeendelea kuimarika kwa miaka minne mfululizo kama ifuatavyo:-

Mwaka	Makisio	Kiasi kilichokusanywa	asilimia	Maelezo
2013/2014	1,475,776,000.00	1,314,377,744.84	89.90	Jitihada zinaongezwa kuhakikisha makisio yanafikiwa
2014/2015	1,812,097,000.00	1,485,836,008.00	82.20	Jitihada zinaongezwa kuhakikisha makisio yanafikiwa
2015/2016	2,380,000,000	1,950,571,155.84	82.98	Jitihada zinaongezwa kuhakikisha makisio yanafikiwa

2016/2017	2,457,310,003.26	2,227,146,930.75	90.63	Jitihada zinaongezwa kuhakikisha makisio yanafikiwa

FEDHA ZA RUZUKU KWA MATUMIZI YA KAWAIDA

MWAKA WA FEDHA	MAKISIO	KIASI KILICHOPOKELEWA (Tshs)	%	SABABU ZA KUTOPATA FEDHA ZOTE
2013/2014	13,616,491,000	9,006,836,502.22	66.13	Serikali kuu kutotuma fedha
2014/2015	16,391,934,000	15,269,232,478.00	93.15	Serikali kuu kutotuma fedha
2015/2016	20,936,282,100.00	20,538,873,496.70	98.10	Serikali kuu kutotuma fedha
2016/2017	23,607,033,922.66	21,393,546,094.91	91.00	Serikali kuu kutotuma fedha

MAFANIKIO YA JUMLA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO NA VIPAUMBELE VYA HALMASHAURI (Ilani ya Uchaguzi)

Kwa kipindi cha 2016/2017 Halmashauri imefanikiwa katika maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

1. Halmashauri yetu imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi yaliyowezesha kupata HATI SAFI ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu za 2014/2015, huu ni mwendelezo wa hati safi kwa mika mitatu mfululizo.
2. **Bajeti ya miradi ya maendeleo imeongezeka kama ifuatavyo**

Mwaka	Kiasi kilichotengwa	Kiasi kilichopokelewa SK	Maelezo
2013/2014	3,734,684,400.00	2,201,340,103	Fedha hazikufika kama ilivyokuwa imekadiriwa kwenye bajeti
2014/2015	2,300,111,000.00	1,008,939,044.34	Fedha hazikufika kama ilivyokuwa imekadiriwa kwenye bajeti
2015/2016	4,287,118,007	5,102,113,273	Fedha za madeni ya miradi ya maji ndizo zilizoongeza mapokezi
2016/2017	7,445,000,193	5,299,040,286	Fedha hazikufika kama ilivyokuwa imekadiriwa kwenye bajeti
2017/2018	6,192,429,000	-	Mapokezi ya mwaka wa fedha bado hayajaanza

TAARIFA ZA KISEKTA

SEKTA YA FEDHA:

Ukusanyaji mapato ya ndani ya Halmashauri

Idara ya fedha imejitahidi kuboresha ukusanyaji mapato na udhibiti wa ndani kwa kuimarisha kitengo cha ukusanyaji mapato, mifumo ya fedha na utoaji taarifa ndani ya wakati. Kwa mwaka wa Fedha ulioisha tarehe 30 Juni 2017, Halmashauri ilikusanya asilimia 90.63 ya makisio ya Mapato ya ndani.

Aidha Halmashauri imetekeleza maagizo ya serikali ya kutumia Mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa Mapato pamoja na kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato hayo.

SEKTA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUALIAJI

Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Miradi ya sekta 9 iliidhinishiwa fedha toka Serikali Kuu .Mapokezi ya fedha na utekelezaji umeanishwa katika jedwali kama ifuatavyo:-

MIRADI ILIYOTOLEWA FEDHA NA UTEKELEZAJI WAKE KUFIKIA JUNI 30, 2017

S/N	MFUKO	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA KUFIKIA JUNI, 30, 2016	% KIASI KILICHOPOKELEWA	MATUMIZI KUFIKIA JUNI 30, 2016	% YA MATUMIZI KWA KIASI KILICHOPOKELEWA
1	MMES/SEDP	130,852,000	0	0	0	0
3	Mfuko wa pamoja wa Afya (HSBF)	505,995,000	505,995,000	100	505,995,000	100
4	Programu ya maji na usafi wa mazingira(RWSSP)	2,822,696,193	1,680,758,345	59.5	1,487,878,782	88.5
5	Mfuko wa barabara(RTF)	1,265,740,000	993,030,386	78.4	993,030,386	100
6	LGDG-CDG	572,005,000	200,017,000	35	200,017,0	100

					00	
7	Mfuko wa Jimbo(CDCF)	40,712,000	40,017,000	98	38,250,439.04	95.6
8	TASAF	2,107,000,000	1,880,022,555	89.2	1,880,022,555	100
9	Mapato ya ndani	1,463,432,000	1,323,547,889.4	90.4	1323547889.4	100
	TOTAL	**8,908,432,193.00**	**6,623,388,175.4**	**74.3**	**6,428,742,051.44**	**97**

KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI

Kitengo kilifanya kazi zake kwa kuzingatia Mpango wa Ukaguzi wa Ndani ambao uliandaliwa kwa kuzingatia Viashiria vya Vihatarishi (Risk based Internal Audit Programme) na kuzingatia Mpango wa Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa Halmashauri wa Mwaka 2016/2017 . Kwa hivyo Ukaguzi ulifanyika ili kuhakikisha Malengo ya Mpango wa Halmashauri yanafikiwa kama ilivyokusudiwa.

Kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 katika Mpango wake wa Mwaka Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kilipanga kufanya Ukaguzi katika maeneo mbalimbali.

Maeneo Makuu ya Halmashauri yaliyofanyiwa Ukaguzi ni:-

- Mfumo wa udhibiti wa Ndani
- Usimamizi wa Mapato
- Usimamizi wa Matumizi
- Usimamizi wa Mishahara
- Usimamizi wa Watumishi
- Usimamizi wa Mikataba
- Usimamizi wa Manunuzi
- Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo
- Usimamizi wa Madeni
- Ukaguzi wa Zahanati na kituo cha Afya
- Mapitio ya Taarifa za Halmashauri

Taarifa za Ukaguzi za kila robo ziliandaliwa na kuwasilishwa katika vikao vya Wakuu wa Idara,Kamati ya Fedha na Mipango,Kamati ya Halmashauri ya Ukaguzi ,Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali,Mkaguzi Mkazi(NAO) , Katibu Tawala wa Mkoa pamoja na Wadau wengine kwa Mujibu wa Taratibu na Miongozo iliyopo.

KITENGO CHA TEKNOLOJIA HABARI NA MAWASILIANO

Kitengo cha TEHAMA kina jukumu la kuhakikisha kuwa sera ya TEHAMA ya taifa na ya Halmashauri zinatekelezwa. Hivyo kitengo kinahakikisha mifumo ya kieletroniki ya kitaifa inayotumika ndani ya Halmashauri inafanya kazi ipasavyo, mifumo hii ni kama ilivyoelezewa hapo chini

Mifumo ya ki-elektroniki ya hesabu; Intergrated Finacial Management Information System (IFMIS)- Epicor 9.05 Kupitia mifumo tajwa usimamizi umerahisishwa na matumizi ya fedha yamedhibitiwa, vile vile na kwa kupitia epicor, Benk kuu imeongeza ufanisi na kurahisisha ulipaji wa fedha kwa kutumia njia ulipwaji wa TISS kwa kuondoa matumizi ya hundi.

Mfumo wa Takwimu wa Elimu msingi na sekondari(BEMIS & PREM); mfumo huu unatumia miundombinu ya mfumo wa Epicor kwa Halmashauri kuunganishwa na wizara ya Elimu; kwa kipindi hiki, kitengo cha TEHAMA kimeshirikiana na idara za Elimu kuhakikisha kuwa taarifa za wanfunzi na shule zinajazwa na kutumwa wizarani.

Mifumo ya utumishi (Human capital Management Information System) Lawson;
mfumo wa HCMIS-Lawson umeendelea kuleta tija katika kusimamia watumishi wote. Mfumo huu unatumika katika kuajiri, kupandisha vyeo watumishi na kuweka sahihi taarifa zote za watumishi kwa ufanisi.

Mfumo wa ukusanyaji wa mapato- Local government Revenue collection Information System (LGRCIS); mfumo wa mapato umeongeza ufanisi katika ukasanyaji wa mapato ya Halmashauri kwani halmashauri imepunguza kwa kiasi kikubwa utumiaji wa vitabu na kutumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa tozo, ushuru na kodi zote.

Mfumo wa Government of Tanzania Hospital Management Information System (GOT-HOMIS) unaendelea kutumika katika Hospitali ya Wilaya kwa Ufanisi mkubwa. Kwa sasa mfumo unaendelea kutumika ktk vitengo vya; mapokezi, keshia, OPD, famasi, maabara, x-ray, theater na wodini. Vitengo vingine vilivyobaki vitaanza mara tu komputa zitakaponunuliwa maana ndo changamoto kubwa iliyopo kwa sasa. Malengo ya GOT-HOMIS ni kurahisisha kusimamia uendeshaji wa shughuli za hospitali, kuweka kumbukumbu za wagonjwa, na kukusanya mapato.

SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

ELIMU MSINGI

Mwaka wa masomo 2016/2017 katika Halmashauri tumekuwa na wanafunzi 32,266 waliosajiliwa (me 16,072 Ke 16,194) ambao waliendelea kupata masomo yao katika shule 59 za serikali na shule 11 za Binafsi zilizopo wilayani mwetu. Shule za Msingi za Bweni za serikali zimefikia 3. Idadi ya walimu katika shule za msingi ni 658 dhidi ya walimu . Aidha matokeo ya Mtihani wa darasa la 7 mwaka 2016 yaliwezesha wanafunzi 1916 (me 898, ke 1018) kuingia shule za sekondari mwaka 2017.

Uandikishaji wa watoto kuingia darasa la kwanza mwaka 2017 ulifikia 5,884 (me 3,005, ke 2,879) ambayo ni sawa na 107% ukilinganisha na 106 % ya mwaka 2016 katika shule 59 za serikali na shule 9 za binafsi. Kiwango cha ufaulu kwa mwaka wa fedha 2016/17 kilikuwa ni 71% ukilinganisha na 70% kwa mwaka 2015/16.

ELIMU SEKONDARARI

Shule za sekondari za serikali ni 12 wakati shule za zisizo za sserikali zipo 9 aidha kuna shule zenye kidato cha tano na sita 05 zikiwemo 02 za serikali na 03 zisizo za serikali. Shule hizi zina jumla ya wanafunzi 8728 wakiwemo wanafunzi to shule za serikali ni 6711 na wanaotoka shule zisizo za serikali 2017.

Shule zetu za serikali zina jumla ya walimu 489 wakiwemo walimu wa Sanaa 370 na walimu wa sayansi 219, aidha kuna upungufu wa walimu wa sayansi 23 tu

Wilaya ina chuo cha ualimu 1, Chuo cha Maendeleo ya Jamii (CDTI) 1 na Chuo Cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) 1. Uwepo wa vyuo hivi vyote ni juhudi za serikali kuhakikisha jamii inapata elimu katika nyanja mbalimbali.

Changamoto kubwa ni upungufu wa miundombinu (kama vile madarasa, nyumba za waalimu, mabweni na maabara), mdondoko wa wanafunzi pamoja na mimba kwa wanafunzi wa kike, mwamko mdogo wa elimu na kukosa mahitaji muhimu kwa wanafunzi wanaotoka familia zenye kipato kidogo

AFYA:

Huduma za afya zimeendelea kutolewa katika zanati 38, vituo vya afya 3 na Hospitali 1 tukitarajia kuongeza huduma zitakapokamilika zahanati 6 nyumba za watumishi 8 zinazoendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali wilayani. Wilaya imeendelea kutoa huduma ya chanjo kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka 5 dhidi ya magonjwa yanayokingika kwa chanjo. Kiwango cha chanjo kwa wastani kimefikia asilimia 108 mwaka 2016/17 dhidi ya wastani wa 102%, mwaka 2015/16. Aidha kiwango cha wanawake wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma kimeongezeka na kufikia 40% kwa mwaka 2016/17 ikilinganishwa na asilimia 37% mwaka 2015/16. Vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi vimepungua kutoka 162 katika kila wanawake 100,000 wanaojifungua kwa mwaka 2015/16 hadi kufikia 102 mwaka 2016/2017. Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 6 mwaka 2015/2016 hadi kufikia vifo 5 katika kila watoto 1000 waliozaliwa hai kwa mwaka 2016/17.

Vita dhidi ya UKIMWI: Hali ya maambukizi ya UKIMWI imeendelea kupungua hadi kufikia 3.8% kufikia mwaka 2016/17 ukilinganisha na 4% mwaka 2015/16. Kamati za kudhibiti

UKIMWI zilizoundwa ngazi ya vitongoji hadi wilaya zimeendelea kujengewa uwezo ili kutoa elimu ya kuzuia maambukizi mapya ya VVU kwa kushirikisha na Asasi mbalimbali za kijamii.

MAJI:

Sekta ya Maji:

Wilaya imeongeza kiwango cha upatikanaji huduma ya maji safi kutoka 62.5% mwaka 2015 hadi 65% kufikia mwezi Juni, 2017. Wilaya ina visima virefu 25, skimu ya maji ya mtiririko 20, malambo/mabwawa 61 na matanki 216 ya kuvunia maji ya mvua. Lengo ni kuinua kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama kutoka 65% cha sasa hadi 80% ifikapo mwaka 2018.

Katika kuhakikisha kuwa miradi iliyojengwa inakuwa endelevu, Wilaya imeratibu na kusajili jumuiya za watumiaji maji 21.

SEKTA ZA KIUCHUMI

BARABARA NA MAWASILIANO:

Wilaya imeendela kufanya matengenezo ya Mtandao wa barabara uliopo wenye urefu wa kilometa 688 zinazounganisha vijiji, kata na tarafa, ukilinganisha na kilometa 454 zilizokuwepo mwaka 2011. Barabara mbili mpya zimefunguliwa kuunganisha Kata za Moita na Kata ya Naalarami na Kata ya Monduli juu na Kata ya Lepurko kupitia Ilimorijo. Aidha katika Mwaka wa fedha 2016/2017 Wilaya imefanya matengenezo ya barabara ya kawaida km 47, Matengenezo ya sehemu korofi km 36 na matengenezo ya muda maalumu km 23.

Ujenzi wa nyumba za makazi ya Watumishi kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) uko kwenye hatua ya umaliziaji hapa Monduli mjini

Mawasiliano ya simu za mkononi yameendelea kubakia asilimia 95% ya eneo la Wilaya. Hata hivyo mipango ya kujenga mifumo ya mawasiliano maeneo Engaruka kupitia Kampuni za Simu za Vodacom na Tigo vimekamilika na utaratibu wa kujenga maeneo mengine ambapo hakuna mawasiliano taratibu zinaendelea kufanyika kupitia Makampuni ya simu za Mikononi. Tunaendelea kuishukuru Serikali yetu kwa kuwezesha ujenzi wa mifumo ya umeme vijijini (REA) awamu ya kwanza ambapo kwa mara ya kwanza umeme umefika Kata za Lolkisale, Lepurko, Selela na Engaruka.

ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:

Ardhi, Maliasili na Mazingira: Wilaya imeweza kuotesha na kupanda jumla ya miti 1,363,541 kupitia vikundi vya watu binafsi na taasisi na vilevile imeendelea kuwasisitiza wananchi kutumia majiko banifu na sola. Hadi kufikia mwezi Julai, 2017 jumla ya kaya 11,947 zinatumia majiko banifu na sola katika kata 14.

Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi: Wilaya inaendelea kutekeleza kazi ya kutengeneza mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote. Hadi kufikia mwezi Julai, 2017 jumla ya vijiji 31 vimekamilisha kazi hiyo sambamba na kuandaa sheria ndogo za vijiji na kwamba kazi hii imesaidia kupunguza migogoro ya ardhi. Na jumla ya hati za kimila 744 zimetolewa na jumla

ya maeneo ya umma 129 yenye ukubwa wa ekari 368 yamepimwa na kuandaliwa hati. Wilaya pia imeongeza juhudi katika usimamizi na uhifadhi wa wanyamapori katika tengefu na hifadhi ya jamii ya Randilen (Randilen WMA). Mathalan Hifadhi ya jamii ya Randilen yenye ukubwa wa Hekta 31,200.68 imekuwa na ongezeko la wanyamapori na uoto wa asili na pia idadi ya watalii imeongezeka kutokana na usimamizi mzuri unaofanywa na vijiji 8 vinavyozunguka hifadhi hiyo vikishirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Honey Guide.

KILIMO, UMWAGILIAJI

Kilimo; Shughuli kubwa za kiuchumi ni kilimo. Katika msimu wa kilimo 2016/2017 jumla ya hekta 27,786 za mazao mbalimbali yanayolimwa zililimwa na jumla ya tani 86,299 zinatarajiwa kuvunwa. Utekelezaji wa malengo ya kilimo katika msimu huu ni asilimia 95%. Wilaya inatarajia kuwa na chakula cha kutosha isipokuwa kwenye kata chache zenye uhaba wa mvua.

Kilimo cha Umwagiliaji: Wilaya imeendelea kupanua eneo la kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya Mto wa Mbu, Selela na Engaruka. Jumla ya hekta 3,200 zinamwagiliwa kati ya hekta 7,700. Skimu 2 za umwagiliaji za Engaruka Juu na Kabambe Selela zimekarabatiwa kwa kusakafia sehemu za mifereji mikuu kwa zegemawe.

Usalama wa Chakula: Kutokana na mvua za vuli na masika, hali ya mazao inaridhisha. Wilaya inatarajia kuvuna jumla ya tani 22,319 za mahindi. Mavuno ya maharage yamepungua kwa zaidi ya asilimia 40 kutokana na ugonjwa na wadudu kwenye zao la maharage.

Pembejeo za Kilimo: Wilaya ilipangiwa jumla ya wakulima 1,000 watakao nufaika na pembejeo za ruzuku, wakulima 350 walichua mbegu , wakulima 140 walichukua mbolea ya kupandia na wakulima 213 walichukua mbolea ya kukuzia, pembejeo hizi zimesambazwa na Mawakala katika kata saba zenye jumla ya vijiji 16. Utaratibu huu wa ruzuku ya pembejeo umesaidia kuongeza mavuno mashambani kwa zao la mahindi kutoka gunia 5-8 kwa ekari hadi wastani wa gunia 15 kwa ekari.

Mapokezi ya chakula

Zoezi la uuzaji wa mahindi yaliyotolewa na serikali ili kupunguza mfumko wa bei ya mahindi. Kazi hii ilifanywa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Monduli. Wilaya ya Monduli ilipokea jumla ya mgawo wa mahindi tani 300 kwa ajili ya kuuza katika maeneo yenye mfumko mkubwa wa bei.
Mahindi yote tani 300 zilinunuliwa na wafanyabiashara kwa ajili ya kusambazwa katika maeneo kusudiwa.

USHIRIKA

Wilaya ina vyama vya Ushirika 25 ambapo idadi ya wanachama imefikia 3519 wanaume 2,088 na wanawake 1385. Vikundi wanachama ni 29 na Taasisi 17. Mitaji iliyowekezwa katika SACCOS inafika Tshs. 852,572,000/= - ikiwa Tsh. 148,356,000/= ni Hisa, Tsh. 562,643,000/= ikiwa ni Akiba na Amana zikiwa Tsh. 141,573,000/=

Wilaya ina idadi ya vyama vya ushirika vya Mazao 5. Vyama 2 vinafanya biashara na Kampuni ya Bia Tanzania – TBL kwa kilimo cha Zao la Shayiri kwa Mikataba. Chama kimoja kinafanya biashara ya Mazao mchanganyiko na ACU Ltd na kimoja kinafanya biashara ya ukodishaji wa majengo yake na mtambo (power Tiller) na kimoja ni sinzia

Village Community Banks (VICOBA): - Idadi Vikundi vilivyo sajiliwa 100 na Uwekezaji wa mitaji unaendelea vizuri ikiwa ni fedha za Hisa, mifuko midogo ya jamii (Elimu na Afya) pamoja na mfuko wa uwezeshaji (kukidhi mitaji midogomidogo kwa wajasiriamali).

MIFUGO

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, idara ya Mifugo na Uvuvi imefanya shughuli zifuatazo;

Kinga ya Magonjwa ya Mifugo: Jumla ya ng'ombe 12,897 wamechanjwa dhidi ya homa ya mapafu (CBPP), 46,854 wamechanjwa dhidi ya Kimeta, 15,476 wamechanjwa dhidi ya ndigana kali na 500 wamechanjwa dhidi ya chambavu. Jumla ya mbuzi 9,576 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu (CCPP), 20,797 wamechanjwa dhidi ya kimeta na mbuzi 846 wamechanjwa dhidi ya sotoka (PPR). Aidha kondoo 20,855 wamechanjwa dhidi ya kimeta, 500 wamechanjwa dhidi ya sotoka (PPR).

Kinga Dhidi ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na magonjwa ya kuku: Jumla ya mbwa 1,235 na paka 192 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa Kichaa cha mbwa na jumla ya kuku 22,370 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kideri, ndui ya kuku na gumboro.

Uboreshaji wa Mifugo ya Asili: Jumla ya ng'ombe majike wa asili 2,427 walipandishwa mbegu Kwa njia ya uhamilishaji na jumla ya madume bora wa nyama aina ya Sahiwal/Boran 86 na mabeberu bora 253 ya nyama aina ya Isiolo yamenunuliwa.

Kuvuna Mifugo ya Asili na Unenepeshaji: Jumla ya mifugo 8,846 ilivunwa na kuuzwa mnadani baada ya kunenepeshwa kwa bei kati ya Tsh. 650,000 hadi 1,200,000. Aidha Wilaya kwa kushirikiana na mashirika yasio ya Serikali imewaunganisha wafugaji binafsi 17 na Vikundi 37 vyenye jumla ya wanachama 185 na taasisi za fedha na kupewa mkopo wa masharti nafuu wa jumla ya shilingi 588,500,000/=

Uboreshaji wa zao la Ngozi: Wilaya imetoa mafunzo ya usindikaji wa zao la ngozi kwa vikundi 4 vyenye jumla ya wanachama 80 ambavyo vinasindika ngozi na kutengeneza bidhaa zinazotokana na ngozi.Vikundi viwili vimefikia kiwango cha kuzalisha bidhaa zinazokaribia kufikia viwango vya ushindani katika soko.

MAENDELEO YA JAMII NA USTAWI WA JAMII:
Wilaya imeweza kutoa misaada kwa wanafunzi 4 wa wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa kuwalipia Ada ya shule na Vifaa vya shule, 2 wako kidato cha tano na 2 chuo cha ufundi FDC. Ushauri wa kitaalamu umeendelea kutolewa kwenye vikundi vya kiuchumi 122 vyenye washiriki 2,447. Mafunzo ya kujengewa uwezo wa usimamizi na uendeshaji wa vikundi vya wajasiriamali yametolewa kwa Wanawake 289. Pia mkopo umetolewa kwa vikundi vya wanawake na vijana 48 wenye thamani ya Tsh. 168,000,000 toka mapato ya ndani ikiwa vikundi vya vijana 16 na wanawake 32.

MWISHO:
Kimsingi Halmashauri imeanza kuona mafanikio ambayo ni kiashiria kizuri kwa manufaa ya wananchi wake. Uendelevu wa mafanikio na mbinu za utekelezaji zilizotumika kufikia mafanikio tunayoyaona iwe ni msingi wa kuanza hatua nyingine. Mafanikio ya utekelezaji wa ilani ndiyo silaha muhimu katika majukumu yaliyoko mbele.

Naomba kuwsilisha.

STEPHEN A. ULAYA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MONDULI